Tanzania Human Rights Defenders Coalition [THRD-Coalition]

P. O. Box 105926 Dar es Salaam, TANZANIA, Mob: +255 783 172394 E-mail: thrddefenders@gmail.com.
Web: **www.thrdc.or.tz**

Ref: THRDC/VOL1/SH/01 **Date: 13th April, 2015**

Mh. Rais wa Jamuhuri ya Muungano
Wa Tanzania,
DAR ES SALAAM.

YAH: MAOMBI YA KUKUSIHI KUTO KUTIA SAINI MISWADA YA SHERIA YA TAKWIMU YA 2015 NA SHERIA YA MAKOSA YA MITANDAO BILA KUFANYIWA MAREKEBISHO

Husika na kichwa cha habari hapo juu.

Mhe. Rais, Mtandao wa watetezi wa haki za binadamu Tanzania, ni muungano wa mashirika zaidi ya 100 yanayo tetea haki za binadamu Tanzania. Mtandao kwa kushirikiana na Wanachama wake pamoja na wasio wanachama tumehuzunishwa na kitendo cha Bunge la Jamhuri ya Muungano kupitisha Muswada wa Sheria ya Takwimu ya Mwaka 2015 na Muswaada wa Sheria ya Makosa ya Mtandaoni bila kuviondoa vifungu vinavyokwenda kinyume na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na Haki za Binadamu kwa Ujumla.

Tunafahamu kabisa dhamira yako ya kuhakishia watanzania wanapata uhuru wa maoni na uhuru wa kufanya shughuli zenye tija kwa Taifa kwa uhuru. Pia tunatumia fursa hii kukupongeza Mhe. Rais Kw kwa jitihada za kuongeza wigo wa ushiriki wa wadau katika mambo mbalimbali kwa kuanzisha progamu mbalimbali za utawala bora, uwazi na ukweli kama vile Open Government Partnership na mengineyo. Kwa misingi hiyo **Mheshimiwa Rais,** tunashauri kabla ya kutia saini miswaada hii upate muda wa kusikiliza kilio cha jamii juu ya ubaya wa sheria hizi kwa mustakabali wa Taifa. Sheria Hizi zikitumika katika utwawala wako zitatia shaka dhamira yako nzuri ambayo umekuwa ukisimamia toka uingie madarakani ya kuongeza wigo na uhuru wa habari na ushiriki wa wadau katika maendeleo ya kitaifa.

Board of Directors:
Dr. Helen Kijo Bisimba, Harusi Mpatani, Martina Kabisama, Tike Mwambipile, Joseph Parsambei, Saed Kubenea, Hamisa Mmanga and Ernest Kimaya.

Mh. Rais, Katika Bunge hili la 19, Serikali ilipeleka Miswada miwili, **Muswada wa sheria ya Takwimu na ule wa Makosa ya Mitandaoni** bila kushirikisha wadau na wananchi kwa kutoa maoni yao. Ili sheria iweze kuwa rafiki na kutekelezeka ushiriki wa wananchi na wadau katika kuitunga ni wa muhimu.

Mtandao kwa kushirikiana na wanachama wake na wadau wengine , tunakuomba na kukusihi Mh. Rais kutokutia saini **Muswada wa sheria ya Takwimu na ule wa Makosa ya Mitandaoni** uliopitishwa na Bunge kwa sababu zifuatazo:

I. Malengo ya Muswada wa Sheria ya Takwimu sio tu kuratibu Takwimu za Kitaifa bali umetoa madaraka Makubwa kwa Ofisi ya Taifa ya Takwimu kama Kitovu cha utoaji wa Takwimu nchini. Maana yake ni kwamba Taasisi zote za Serikali, Mashirika Binafsi, Taasisi za Elimu ya Juu, Vyuo vikuu na Taasisi za Utafiti hazitokuwa na uhuru wa kutoa matokeo ya tafiti wanazozifanya bila ya kibali au ridhaa ya Ofisi ya Takwimu.

II. Muswada wa Sheria ya Takwimu umezitambua taarifa na takwimu zote nchini hata kutoka Taasisi Binafsi kuwa katika mfumo wa Kitaifa wa Takwimu unaoratibiwa na Ofisi ya Takwimu. Utaratibu huu haukubaliki na ni hatari kwa mustakabali wa Taifa.

III. Muswada wa Sheria ya Takwimu unazitaka taasisi zote zikiwemo binafsi kuwajibika kwa Ofisi ya Takwimu na kupata ridhaa ya Mkurugenzi Mkuu wa Ofisi ya Takwimu kutoa taarifa za kitakwimu; Mfano, Kifungu cha 20 (2) kinasema "Takwimu zote zitakazotolewa na wakala (Kwa mujibu wa sheria hii wakala ni taasisi binafsi, mashiirika ya utafiti, wadau wa maendeleo, watumiaji au wazalishaji wengine wa Takwimu) zinapaswa kuwa zinakidhi matakwa ya Ofisi ya Takwimu na kuidhinishwa na Mkurugenzi Mkuu".

IV. Muswada wa Sheria ya Takwimu umeweka adhabu kali na kubwa kwa Vyombo vya Habari, Asasi za kiraia, Taasisi za Utafiti na vyuo vya Elimu ya Juu vitakavyotenda makosa yalianishwa katika Sehemu ya Tatu ya Sheria. Mfano wa makosa yanayotishia shuguhuli za utafiti hapa nchini pamoja na adhamu zifuatazo; Kifungu cha 37 cha Sheria hii kinasema mtu yoyote au taasisi itakayotoa takwimu au taarifa za kitafiti ambazo Ofisi ya Takwimu inaziona ni za uongo anatenda kosa na kustahili kifungo cha miezi sita na faini isiyopungua million mbili. Vifungu hivi ni hatari kwa kuwa hakuna utaratibu unaoweza tambua kuwa tafiti ya taasisi fulani ni ya uongo, bali nafasi hii itatumika na Serikali na baadhi ya watawala kuminya uhuru wa taasisi binafsi kutoa taarifa mbalimbali za kitafiti zikiwemo vyuo vikuu.

V. Muswada wa Sheria ya Takwimu pia umelenga kuua Uhuru wa Habari kwa kuweka adhabu ya faini isiyopungua milioni 10 na kuifungo cha miaka miwili kwa kuchapisha taarifa au takwimu za uongo au za upotoshaji. Wakati Taifa linahubiri kuzingatia Uhuru wa Vyombo vya Habari na haki ya kupata habari.

VI. Kwa ujumla Muswaada huu umekuja kuzima kazi zote za kitafiti zinazofanywa na taasisi binafsi, vyuo vikuu na vyombo vya habari. Mfano tafiti zozote zinazofanywa na vyuo vikuu, taasisi za kitafiti kama vile REPOA, ESRF, REDET, NIMR; Mashirika yasiyo ya kiserikali kama vile

Board of Directors:
Dr. Helen Kijo Bisimba, Harusi Mpatani, Martina Kabisama, Tike Mwambipile, Joseph Parsambei, Saed Kubenea, Hamisa Mmanga and Ernest Kimaya.

LHRC, TWAWEZA, HAKIELIMU, SIKIKA, HAKIARDHI na nyingine nyingi ni lazima sasa zipite chini ya usimamizi wa Ofisi ya Takwimu.

VII. Pia Muswaada wa Sheria hii una utofauti mkubwa kwa ule ulioandikwa kwa lugha ya Kiswahili na lugha ya Kingereza. Mfano, adhabu karibu zote zilizotolewa zinatofautiana toka toleo la Kiswahili na la Kiingereza.

VIII. **Tunakushauri Mhe Rais** kutafakari upya changamoto zilizoanishwa katika muswada wa sheria ya Makosa ya Mitandao ya 2015. Sheria hii kama imeletwa kwa malengo mazuri ya kupinguza matumizi mabaya ya mitandao, ingekuwa busara ushiriki wa umma wa Watanzania kabla ya kuupitisha.

IX. Muswaada wa Sheria hii ya makosa ya Mitandao itabinya kwa kiasi kikubwa uhuru wa wananchi kuwasilina na kupashana habari kama itasainiwa bila marekebisho na kuwa sheria. Ni dhahiri sheria hii imelenga kufuta kabisa matumizi ya mitandao ya kijamii kama vile Facebook, WhatsApp, JamiiForums, twitter, blogu n.k. Kupitishwa kwa sheria hii bila kufanyiwa marekebisho kutasabisha watanzania wengi kuwekwa hatiani bila sababu, lakini pia kutaondoa kabisa uhuru wa habari nchini.

X. **Mh. Rais,** katika Muswaada huu wa sheria ya makosa ya mitandaoni Mamlaka waliyopewa wakuu wa Vituo vya Polisi, Waziri mwenye dhamana yatawaumiza watanzania wengi, ni vyema suala hili lingeangaliwa kwa jicho la pili ili Mhimili wa Mahakama uweze kupata heshima yake na kuliondoa suala hili kwa Jeshi la Polisi ambalo limekuwa likilalamikiwa na wanachi

Kutokana na sababu hizo tajwa, tunakuomba na kukusihi Mh. Rais kutotia saini mpaka pale bunge litakapofanya marekebisho na kuboresha mapungufu yaliyo ainishwa na wadau mbalimbali. Miswaada ya Sheria hizi zinavunja haki nyingi za kikatiba na za kibinadamu.

Barua hii imeletwa kwako na Mtandao kwa niaba ya Mashirika ya Kutetea Haki za Binadamu na Taasisi za Habari zilizoorodheshwa katika barua hii.

Mh Rais, hii ndio orodha ya Mashirika 100 yanayoleta Ujumbe huu kwako

1. LHRC
1. LEWOPAC
2. WOTE SAWA
3. KASULU LEGAL AID
4. HAKI MADINI
5. JOURNARIGHT
6. SIKIKA
7. ZAFELA

Board of Directors:
Dr. Helen Kijo Bisimba, Harusi Mpatani, Martina Kabisama, Tike Mwambipile, Joseph Parsambei, Saed Kubenea, Hamisa Mmanga and Ernest Kimaya.

8. CENTER FOR HUMAN RIGHTS PROMOTION
9. YOUTH TO YOUTH
10. UNDER THE SAME SUN
11. TUFAE
12. JUKWA LA KATIBA
13. MISA- TAN
14. MUSODEO
15. TCIB
16. ZLSC
17. PINGO's FORUM
18. TGNP Mtandao
19. TAWLA
20. MIKONO YETU
21. WORLD YOUTH ALLIANCE
22. ABC Foundation
23. UTPC
24. TPCF
25. WASHEHABISE TANZANIA
26. MTWARA PARA LEGAL
27. SAHRINGON
28. HAKI ZA BINADAMU MBEYA
29. TAMWA
30. TAS
31. HALI HALISI PUBLISHER
32. MOIPAC
33. KIVULINI
34. Kigoma Women Development (KIWODE)
35. Shamsia Women Group (CBO)
36. DUNGONET (Ngo's Network for Dodoma Urban)
37. Better Life (NGO)
38. Rural Women Development Iniatiavites (RUWODI)
39. Bethania empowerment and suport (BEST)
40. Mbeya Women
41. Tanzania Youth Potential Association
42. Tanzania Centre for Research and Information on Pastoralism
43. Haki za Binadamu Mbeya
44. Tanzania Network of legal providers Ltd (TANLAP
45. Tanzania Patnership Development Organization
46. SANA
47. PAICODEO

TUJIBU Coalition

Board of Directors:
Dr. Helen Kijo Bisimba, Harusi Mpatani, Martina Kabisama, Tike Mwambipile, Joseph Parsambei, Saed Kubenea, Hamisa Mmanga and Ernest Kimaya.

THRD-Coalition

Board of Directors:
Dr. Helen Kijo Bisimba, Harusi Mpatani, Martina Kabisama, Tike Mwambipile, Joseph Parsambei,
Saed Kubenea, Hamisa Mmanga and Ernest Kimaya.